

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**Enyi Maafisa wa Jeshi la Pakistan! Mutamjibu Nini Mwenyezi Mungu (swt), Pindi Mwenyezi Mungu (swt) Atakapowahisabu kwa Kutojiletea Nafsi Zenu, Vifaru Vyenu, Silaha Zenu na Makombora Yenu katika Hatua ya Mara moja, Kuutokomeza Uvamizi Halifu wa Kiyahudi, kwa Kuitikia Vilio vya Watoto wa Palestina?!**

(Imetafsiriwa)

Katika kipindi cha siku mbili za maumivu, Waislamu arubaini na nne wakiwemo watoto wameuawa shahidi, huku zaidi ya mia tatu wakijeruhiwa, kutokana na mashambulizi ya kikatili ya wanajeshi wa Kiyahudi kwa Ukanda wa Gaza, Palestina, ambako hata hospitali haikusazwa. Kutoka Indonesia hadi Morocco, Umma wa Kiislamu unajibu kwa hasira bila ya kutulia, kwa kulazimishwa na fungamano lenye nguvu la udugu wa Kiislamu. Hata hivyo, watawala walio juu ya shingo za Ummah, wakiwemo watawala wa Pakistan, wameganda, ila kwa domo tupu. Watawala wa Waislamu wanaitikia kana kwamba ulipuaji huu wa mabomu hauko juu ya nyumba za Waislamu wa Palestina, Ardhi Iliyobarikiwa, ardhi ya Kibla cha Kwanza, Isra'a na Miraj ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw). Hawachukui hata hatua kama ambavyo wangepaswa, kana kwamba uharibifu huu wa wazi ni mazoezi tu ya kijeshi, yenye kuangamiza miti, ndege, wadudu na vichaka, katika ardhi, mbali, mbali kabisa. Baya zaidi, watawala hao wanawaomba hata hao hao walaghai na magaidi, dola za Kimagharibi na ile inayoitwa 'jumuiya yao ya kimataifa,' ambayo Mayahudi wanaitegemea, huku wakitekeleza uhalifu huu, bila kuingiliwa.

**Enyi Wanajeshi wa Pakistan!** Munaona kwamba wakati wowote uwepo wa Mayahudi unapotaka, huwaosha Waislamu wa Palestina kwa damu yao wenyewe. Je! Umbile hili la Kiyahudi halipaswi kuogope kwamba kutokana na uhalifu wake, lau tu hata jeshi moja la Waislamu litasonga, itasababisha mwisho uwepo wake, licha ya kusaidiwa na dola za Magharibi? Je, halipaswi kuogopa na kukoma, kwa sababu limezungukwa na Ardhi za Waislamu na majeshi yao? Hapana! Umbile la Kiyahudi haliogopi mitiko wa kijeshi, kwa sababu linajua kwamba watawala wa Waislamu ni vibaraka wa ukoloni, ambao kamwe hawatasonga dhidi yake. Badala yake, wanajipanga kwa safu ili kuhalalisha uwepo wake! Basi mpaka lini mutawaruhusu wale wasiojali utakatifu wa Al-Aqsa, Ardhi ya Waislamu na damu za Waislamu wakuziieni?!

**Enyi Maafisa wa Vikosi vya Wanajeshi vya Pakistan! Enyi Watoto wa Salahudin!** Ving'oeni viti vya enzi vya watawala hawa wasio na soni na uongozi wa khiyana. Toeni Nusrah kwa ajili ya Khilafah kwa Njia ya Utume, ambayo itaangamiza uvamizi ya Mayahudi. Al-Masjid Al-Aqsa unasubiri mngurumo wa vifaru vyenu vya ukombozi, manuari, mizinga na bunduki. Unasubiri takbira za askari wenu wachanga na SSG, kabla ya kuswali, baada ya ushindi, ndani ya maeneo yake yaliyo barikwa. Hivyo basi toeni Nusrah yenu kwa ajili ya Khilafah, ili mupaze takbira huku mukiongozwa katika Jihad, na Khalifah wa Waislamu. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ تَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجْتُمُ] ]

“Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni” [Surah Al-Baqarah 2:191].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**